




Jina :NAMBARI.....DARASA.....TAREHE.....

SAHIHI.....



<i>Date done</i>	
<i>Invigilator</i>	
<i>Date returned</i>	
<i>Date revised</i>	

JANUARI 2019

KIDATO CHA NNE

FASIHI YA KISWAHILI

102/2.3

MUDA : MASAA MAWILI NA NUSU.

MAAGIZO

- Andika jina lako na nambari ya mtahini katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Tia sahihiyako kasha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Jibu maswali **manne** pekee.
- Swali la kwanza ni la **lazima**.
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani, riwaya, tamthilia, fasihi simulizi na hadithifupi.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

Swali	alama

**SEHEMU A: LAZIMA: SHAIRI
WASIA**

Huno wakati mufti, vijana nawausia
Msijejotalaiti, mkamba sikuwambia
Si hayatisimamati, vijana hino dunia
Uonapovyang'aria, tahadhari vitakula

Japo aula kushufu, namachoni vyavutia
Dunia watu dhaifu, yaugua nasikia
Vijana nawasarifu, falau mkisikia
Uonapovyang'aria, tahadhari vitakula.

Jepusheni na zinaa, mlale penye sheria
Msijeandama baa, makaa kujipalia
Jepusheni na zinaa, madhara kukadiria
Uonapovyang'aria, tahadhari vitakula.

Ngawa waone wazuri, nadhifu kukuvalia
Wajimwaie uturi, na mapoda kumichia
Si mlango nyumba nzuri, ngia ndani shuhudia
Uonapovyang'aria, tahadhari vitakula.

Wawapi leo madume, anasa walopapia?
Wamepita jaumeme, leo yao sitoria
Shime enyi wanashime, bora kumcha Jalia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula

Nambie faida gani, nambie ipi fidia
Upatayo hatimani, waja wakikufukua
Ila kufa kama nyani, kasoro yako mkia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

Vyatiririkatariri, vina vyanikubalia
Alo bora mshairi, pa tamu humalizia
Nahitimisha shairi, dua ninawapigia
Uonapovyang'aria, tahadhari vitakula.

Ewe Mola mtukuka, si shaka wanisikia
Wakingie wanarika, na anasa za dunia
Amina wangu Rabuka, dua yangu naishia
Uonapovyang'aria, tahadharivitakula.

MASWALI:

- a) Ni ujumbe gani wanaopewa vijana kupitia shairi?. (alama 4)
- b) Bainisha tamathali mbili za usemi katika shairi hili. (alama 2)
- c) Eleza bahari ya shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 2)
- i) idadi ya vipande katika mshororo
- ii) mpangilio wa vina katika beti.
- d) Eleza mbinu zozote mbili za kishairi zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)
- e) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari (alama 4)
- f) Eleza toni ya shairihili. (alama 1)
- g) Tambua: (alama 2)
- i) Nafsineni
- ii) Nafsinenewa
- h) Eleza umuhimu wa mbinu ya kimtindo iliyotumika katika ubeti wa tano. (alama 2)
- i) Eleza maana ya msamiati: 'aula' (alama 1)

SEHEMU B: RIWAYA

CHOZI LA HERI (Alama 20)

2. Riwaya ya chozi la heri inaonyesha matukio halisi katika jamii. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea mifano mwafaka

SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE (ALIFA CHOKOCHO NA DUMU KAYANDA)

TUMBO LISILOSHIBA (S. A MOHAMMED)

3. "Hakuna aliyeweza kukitegua kitendawili chenyewe lakini..."

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Tambua tamathali ya usemi iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)

- c) Fafanua chanzo na hatima ya kitendawili kinachorejelewa katika dondoo hili. (alama 10)
- d) Eleza wasifu wa warejelewa katika dondoo hili. (alama 4)

SEHEMU YA E: FASI HI SIMULIZI

JIBU SWALI LA 7 AU 8

4. a) Ulumbi ni nini? (alama 2)
- ii) Ulumbi hutekeleza majukumu gani katika jamii? (alama 5)
- iii) Fafanua mambo **manne** yanayomfanya mtu awe mlumbi bora. (alama 8)
- b) Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihisimulizi. (alama 5)
5. a) i) Eleza sifa **sita** za maghani. (alama 6)
- ii) Fafanu aina zozote **nne** za maghani. (alama 4)
- b) i) Fafanua majukumu **manne** ya hurafa katika jamii. (alama 4)
- ii) Eleza vipengele **sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. (alama 6)